# Mshauri wa ujenzi machinjio Vingunguti awekwa kiti moto

**Na CHRISTOPHER LISSA**

MKUU wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, amemtaka mkandarasi mshauri wa ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti, kuripoti ofisini kwake ili kujieleza kuhusu kuchelewa kutoa ushauri wa mipaka ya eneo la mradi huo.

Mkandarasi mshauri katika mradi huo unaotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), ni Cons Africa Ltd.

Pia, ameishauri NHC kuhakikisha inaongeza kasi ya ufuatiliaji wa mabati ya kuezekea machinjio hayo, ambayo inadaiwa yameagizwa kutoka nje ya nchi.

Alitoa maagizo hayo Dar es Salaam, jana, alipofanya ziara ya kukagua miradi ya kimkakati, ambayo ni ujenzi wa machinjio hayo na ujenzi wa soko la Kisutu.

Akiwa katika machinjio hayo, Mjema alieleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi, ingawa alishangazwa na changamoto ndogo ndogo zinazofanya baadhi ya hatua muhimu za ujenzi, hususan uezekaji na kutobainishwa kwa mipaka kamili ya eneo la mradi.

"Nimeambiwa ripoti ya ujenzi huu imekabidhiwa kwa wakubwa. Rais Dk. John Magufuli aliagiza ujenzi ukamilike Desemba 31, mwaka jana, lakini mpaka sasa bado na nimeelezwa kuwa katika ripoti yao, NHC wameomba siku 180 zaidi ili kukamilisha ujenzi, hili liko kwa wakubwa watalitolea amuzi," alisema.

Mkuu huyo wa wilaya alibainisha kuwa, NHC pia wamemueleza kuwa, kinachochelewesha kuezeka ni kutokana na mabati kuagizwa nje ya nchi, kwa sababu hapa nchini hakuna kiwanda kinachozalisha mabati yenye kiwango kinachohitajika kuezekea mradi huo.

"Sasa nawahimiza NHC wafuatilie mabati hayo ili tuezeke jengo hili. Tuko nyuma sana ya muda," alisema.

Kuhusu mshauri wa mradi huo, Cons Africa Limited, Mjema alisema anatakiwa kubainisha mipaka kamili ya eneo hilo ili kumwezesha mkandarasi kujenga miundombinu, hususan ya kupitishia uchafu.

"Kazi zingine za nje ya jengo zimesimama kwa sababu NHC hawajaelekezwa. Namuagiza mshauri wa mradi aje ofisini kwangu Jumatano (kesho)," alisema.

Akiwa katika Soko la Kisutu, Mjema alimtaka Mkandarasi, Kampuni ya Mohammed Builders Limited, kuongeza nguvu kazi na kukamilisha ujenzi kwa wakati.

"Mkataba unamtaka akabidhi jengo Agosti, mwaka huu, lakini ni mbali mno. Tangu mwaka jana, alipoanza ujenzi wa jengo hili lenye ghorofa tano, yuko asilimia 32 tu ya ujenzi, yaani amejenga ghorofa moja. Nataka aongeze kasi na akamilishe angalau Julai, mwaka huu," aliagiza.

Mradi wa Machinjio ya Vingunguti, unagharimu sh. bilioni 12 na unatarajiwa kuwa na tija kubwa kwa taifa, hususan kuinua kiwango cha ubora wa nyama na ngozi pamoja na kuingiza pato kwa nchi.

Hivi karibuni, Uhuru ilizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Dk. Maulid Banyani na kusema taarifa ya kiufundi na kitaalamu kuhusu maendeleo ya ujenzi wa machinjio hayo, imekabidhiwa kwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi.

Taarifa hiyo pia inahusu sababu za kuchelewa kumalizika kwa ujenzi wa mradi.

Lukuvi alitaka sababu hizo zielezwe wazi na ziwe za msingi ili baada ya hapo, amtaarifu Rais Dk. Magufuli kuhusu ucheleweshwaji huo.

Dk. Banyani alisema mabati ya machinjio hayo yameagizwa nchini Kenya, baada ya Tanzania kutokuwa na kiwanda kinachozalisha mabati yenye ubora huo

UJUMBE WA MTAWALA

Scanned by CamScanner

# Mpina aagiza meli iliyokamatwa kwa uvuvi haramu kuondolewa

Na Mwandishi Wetu, Mtwara

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amemtaka mmiliki wa meli ya Buah Naga 1 iliyokamatwa kwa makosa ya uvuvi haramu katika ukanda wa Bahari Kuu kuiondoa haraka meli hiyo katika Bandari ya Mtwara ili kupisha shughuli zingine za Serikali kuendelea, kwani Mahakama tayari ilishatoa hukumu dhidi ya kesi hiyo.

Akizungumza mara baada ya kuitembelea meli hiyo inayomilikiwa na Raia wa Malaysia katika Bandari ya Mtwara, Waziri Mpina alisema kukamatwa kwa meli hiyo na kisha Mahakama kutoa hukumu ya kifungo cha miaka 20 jela au kulipa faini ya sh. bilioni 1 ni uthibitisho kuwa Serikali ya awamu ya tano haina mzaha katika kusimamia rasilimali zake zikiwemo za uvuvi.

Waziri Mpina alisema meli hiyo ya Buah Naga 1 ni ya pili kukamatwa na Serikali ikifanya uvuvi haramu katika Bahari Kuu, ambapo meli nyingine ya Tawariq 1 ilikamatwa mwaka 2009 ikifanya uvuvi haramu na aliyekuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dkt. John Pombe Magufuli.

Mpina alisema baada ya Dkt. Magufuli kukamata meli hiyo miaka 10, baadae ndipo Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Magufuli, ikakamata tena meli hiyo na kuitangazia dunia kuwa Tanzania imekataa kuwa shamba la bibi la kila mtu kuja kufanya anachotaka.

Mpina alisema adhabu iliyotolewa na Mahakama inatoa fundisho na ujumbe kwa wamiliki wa meli na vyombo vingine vinavyotumika kufanya shughuli za uvuvi kuzingatia sheria za nchi.

Alisema Serikali ya Tanzania itaendelea kufanya doria na operesheni katika ukanda wa Bahari Kuu na kudhibiti meli zote za kigeni zilizozoea kuja kuvua katika maji ya Tanzania bila kufuata sheria na badala yake kuvua uvuvi usio endelevu kama kuwavua papa na kisha kutupa miili yao baharini baada ya kuondoa mapezi yake.

Desemba 2018 Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Rushwa Kanda ya Mtwara iliwahukumu watu watatu wakiwemo raia wawili wa kigeni na Mtanzania mmoja kifungo cha miaka 20 jela kila mmoja au kulipa faini ya sh. bilioni 1 baada ya kukamatwa wakifanya uvuvi haramu katika ukanda wa Bahari Kuu Januari mwaka huu.

Watu hao walikamatwa katika 'Operesheni NMATT' iliyokuwa inaendeshwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola katika Meli ya Buah Naga 1 ya nchini Malaysia wakiwa na kilo 90 za mapezi ya papa bila kuwa na miili yake kinyume cha Sheria kati ya mikoa ya Lindi na Mtwara na kutakiwa kulipa faini ya sh.milioni 770 ambapo walikwenda mahakamani kupinga adhabu hiyo.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Rushwa Kanda ya Mtwara, Lilian Mashaka ambapo washtakiwa hao walikiri kutenda kosa hilo ambapo kwa mujibu wa kesi hiyo ya Uhujumu Uchumi Namba 2 ya mwaka 2018, Mahakama hiyo imewakuta na hatia na kutoa adhabu hiyo.

Jaji Mashaka amewataja washtakiwa waliohukumiwa kuwa ni pamoja na Nahodha wa meli hiyo, Han Ming Chuan, Raia wa China, Mmiliki wa Meli hiyo, Dato Seri Lee Raia wa Malaysia na Wakala wa Meli hiyo, Abubakar Salum, Raia wa Tanzania.

Washtakiwa hao walikutwa na hatia baada ya kukiuka Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ikisomwa pamoja na Kanuni ya 66 ya Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu za mwaka 2009 pamoja na aya ya 26 ya jedwali la kwanza na kifungu cha 57 (1) na 60 vya sheria ya uhujumu uchumi na udhibiti wa makosa ya kupanga sura ya 200 na marejeo yake ya mwaka 2002.

Kesi hiyo iliyosimamiwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Peter Maugo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya na Wakili wa Serikali, Wankyo Simon ambapo pamoja na hukumu hiyo, Mahakama Kuu imeamuru meli hiyo pamoja na samaki waliopo akabidhiwe mmiliki wake na mapezi hayo yateketezwe kwa moto na Serikali.

Mwishoni mwa mwaka jana Bunge la Tanzania lilipitisha Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Chakula Duniani wa kupambana na kuzuia uvuvi haramu kupitia Bandari za nchi wanachama ambapo Spika wa Tanzania, Job Ndugai alitaka juhudi zaidi kufanyika kulinda rasilimali za uvuvi kwani ikiwa hazitasimamiwa vizuri zitatoweka.

Scanned by CamScanner

kusababisha usumbufu kwa mabasi yanayotumia kituo hicho.

# Mil. 800/- kujenga machinjio Kibaha

Na Julieth Mkireri, KIBAHA

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha, mkoani Pwani, inajenga machinjio ya kisasa kwa gharama ya Sh. 804,309,600 ambayo itakuwa na uwezo wa kuchinja zaidi ya ng'ombe 100 kwa siku.

Katika mwaka wa fedha 2018/2019 halmashauri hiyo, ilitenga kiasi cha Sh. 945,059,000 kwa ajili ya ujenzi wa machinjio ya kisasa awamu ya kwanza.

Hayo yamebainishwa jana mjini hapa na Ofisa Uhusiano wa Halmashauri hiyo, Innocent Byarugaba, alipozungumza na Nipashe.

Byarugaba alisema kati ya fedha hizo Sh. 140,750,000 ni kwa ajili ya usimamizi na ushauri na Sh. 804,309,600 ni kwa ajili ya machinjio hiyo katika eneo la Mtakuja Kata ya Pangani.

Machinjio hiyo ambayo inajengwa na mkandarasi M/S Petra Construction co.L.td, ujenzi wake ulianza Aprili 2019 na alitarajiwa kukamilisha kazi Novemba 2019.

Byarugaba alisema kuwa kwa awamu ya kwanza kazi za miradi huo zimefikia asilimia 90, na malipo yaliyofanyika hadi sasa ni Sh. 459,279,586.47.

Alisema, katika utekelezaji wa mradi huo zipo changamoto ambazo zimesababisha mkandarasi kushindwa kukamilisha kwa wakati, ikiwamo mvua zilizonyesha katika kipindi cha mkataba zilizosababisha kasi ya ujenzi kupungua.

Changamoto nyingine ilielezwa ni kubadilika kwa eneo la ujenzi wa machinjio na mipaka kati ya msitu wa hifadhi ya Ruvu na Halmashauri ya Mji Kibaha.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, kukamilika kwa mradi huo kutawezesha kuimarisha mapato ya halmashauri, kupitia uuzaji wa ngozi, damu na ushuru wa kuchinja.

Scanned by CamScanner

# Waziri aagiza meli iliyokamatwa uvuvi haramu itolewe bandarini

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amemtaka Mmiliki wa Meli ya Buah Naga I, iliyokamatwa kwa makosa ya uvuvi haramu katika ukanda wa Bahari Kuu, kuiondoa haraka meli hiyo kwenye Bandari ya Mtwara, ili kupisha shughuli zingine za serikali.

Amesema meli hiyo inapaswa kuondolewa bandarini huko kwa kuwa tayari mahakama ilishatoa hukumu dhidi ya kesi hiyo.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo iliko meli hiyo inayomilikiwa na raia wa Malaysia, Waziri Mpina alisema jana kuwa kukamatwa kwa meli hiyo na kisha mahakama kutoa hukumu ya kifungo cha miaka 20 jela au kulipa faini ya Sh. bilioni moja, ni uthibitisho kuwa serikali ya awamu ya tano haina mzaha katika kusimamia rasilimali zake, zikiwamo za uvuvi.

Waziri huyo alisema meli hiyo ni ya pili kukamatwa na kuchukuliwa hatua na serikali, kutokana na kufanya uvuvi haramu katika Bahari Kuu ndani ya miaka 10, ya kwanza ikiwa ni Tawariq I, iliyokamatwa mwaka 2009 na aliyekuwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Dk. John Magufuli, sasa Rais wa Tanzania.

Mpina alisema baada ya Dk. Magufuli kukamata meli hiyo miaka 10, baadaye, serikali anayoiongoza imekamata tena meli nyingine na kuitangazia dunia kuwa Tanzania imekataa kuwa shamba la bibi la kila mtu kuja kufanya anachotaka.

Alisema adhabu iliyotolewa na mahakama inatoa fundisho na ujumbe kwa wamiliki wa meli na vyombo vingine vinavyotumika kufanya shughuli za uvuvi, kuzingatia sheria za nchi.

Waziri huyo alisema serikali itaendelea kufanya doria na operesheni katika ukanda wa Bahari Kuu na kudhibiti meli zote za kigeni zilizotumika kuvua katika maji ya Tanzania bila kufuata sheria.

Alisema uvuvi huo usiozingatia sheria za nchi, si endelevu kutokana na wavuvi kuvua papa na kisha kutupa miili yao baharini baada ya kuondoa mapezi.

Desemba 2018, Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Rushwa Kanda ya Mtwara, iliwahukumu watu watatu wakiwamo raia wawili wa kigeni na Mtanzania mmoja, kifungo cha miaka 20 jela kila mmoja au kulipa faini ya Sh. bilioni moja baada ya kukamatwa wakifanya uvuvi haramu katika ukanda wa Bahari Kuu Januari mwaka huo.

Watu hao walikamatwa katika 'Operesheni NMATT', iliyokuwa inaendeshwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola.

Watu hao walikamatwa wakiwa kwenye meli ya Buah Naga I ya Malaysia wakiwa na kilo 90 za mapezi ya papa bila kuwa na miili yake, kinyume cha sheria.

Pia mwishoni mwa mwaka jana, Bunge la Tanzania lilipitisha Azimio la Mkataba wa Kimataifa wa Shirika la Chakula Duniani wa kupambana na kuzuia uvuvi haramu kupitia bandari za nchi wanachama, Spika Job Ndugai akitaka juhudi zaidi kufanyika kulinda rasilimali za uvuvi akisisitiza kuwa endapo hazitasimamiwa vizuri, zitatoweka.

Scanned by CamScanner